

Njoo, Unifuate Shughuli za

Kwa ajili ya jioni ya nyumbani au kujifunza maandiko—au kwa ajili ya burudani tu!

KWA AJILI YA MOSIA 4–6

Tembea katika Nyayo Zake

Mfalme Mosia alishika amri na “alitembea katika njia za Bwana” (Mosia 6:6). Kwenye kipande cha karatasi, chora kufuatisha mguu wako na kata umbo hilo. Andika kwenye mchoro wa mguu wako jinsi unavyoweza kumfuata Yesu. Weka mchoro wa mguu wako mahali ambapo unaweza kufuata mfano wa Yesu Kristo.

Kwa ajili ya watoto wadogo:

Nendeni kwenye matembezi. Acha mtoto wako afanye zoezi kukanyaga pale ulipokanyaga. Zungumza kuhusu jinsi tunavyoweza kumfuata Yesu Kristo kwa kufanya mambo ambayo Yeye alifanya, kama vile kuwasaidia wengine na kubatizwa.



KWA AJILI YA MOSIA 7–10

Mfuate Nabii

Amoni alifundisha kwamba manabii wanaweza kuona vitu vitakavyokuja (ona Mosia 8:16–17). Nenda kwenye ukurasa wa 2 ili usome ujumbe wa Rais Nelson kutoka kwenye mkutano mkuu. Alitufundisha nini? Chora picha kuhusu jambo hilo alilofundisha na ututumie kwenye Rafiki.

Kwa ajili ya watoto wadogo:

Imba “Follow the Prophet” (*Kitabu cha Nyimbo za Watoto*, 110–11) pamoja na watoto wako. Kila mara mnapoimba neno *nabii*, onesho picha ya nabii.



VIELELEZO NA KATY DOGRILL

KWA AJILI YA MOSIA 11–17

Nuru Gizani

Abinadi alifundisha kwamba Yesu Kristo ndiye “nuru isiyo na mwisho, ambayo haiwezi kutiwa giza” (Mosia 16:9). Ficha chombo katika nyumba. Zima taa na uache kila mtu ajaribu kukipata gizani. Kisha ficha chombo na mjaribu kukipata kama taa zimewashwa au kwa kutumia kurunzi. Ni njia gani ilikuwa rahisi? Je, ni kwa jinsi gani Yesu hutusaidia kama vile nuru ilivyokusaidia?

Kwa ajili ya watoto wadogo:

Acha mtoto wako afanye zoezi la kuwasha na kuzima kurunzi au taa. Kisha zungumza kuhusu jinsi ambavyo Yesu Kristo ni nuru ambayo kamwe haiwezi kufichwa au kuzimwa.



KWA AJILI YA MOSIA 18–24.

Mioyo Inafumwa katika Umoja

Alma alitufundisha kuwa na “mioyo yetu kuunganishwa pamoja katika umoja na upendo” (Mosia 18:21). Hiyo inamaanisha tunapaswa kufanya kazi pamoja na kuonyesha upendo kwa wengine. Tengeneza mlolongo wa mioyo ili kukukumbusha! Kata kiasi cha mioyo ya karatasi na uandike jina la mwanafamilia katika kila moja. Toboa tundu katikati ya kila moyo na upitisho uzi ili mioyo iwe imeunganika. Ning'iniza uzi wako wa mioyo mahali utakapoweza kuuona kila mara!

Kwa ajili ya watoto wadogo:

Muulize mtoto wako kitu kimoja wanachopenda kuhusu kila mtu katika familia. Mwambie mtoto wako kitu fulani ambacho wao hufanya ambacho huonyesha upendo kwa wengine!

